**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**24 Mei 2008**

**Waliohudhuria**
Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Ally Salum
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Markus Weise
Mussa Omari
Paulo Atibu Hatibu
Sudi Saidi Ramadhan

**Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund**
Elaine aliandika barua kutoa maelezo kwa shule kuhusu mradi.

Wakati wa wiki Elaine alijaribu kuwasiliana na mwalimu mkuu wa Mbondole Secondary School lakini hakujibu, basi aliwatumia message kwa wanachama kusema tusiendelee na mpango wa kwenda pale kama kundi kubwa leo. Juma na Ally Athman walienda kule alhamisi. Walienda na baisikeli na walichukuwa zaidi ya masaa matatu kwenda na tena kurudi. Waliwapabarua. Waliongea na mwalimu Abdallah Kilonda ambaye alipenda kushirikiana katika mradi. Alisema kwamba walimu wakuu (Ngulangwa – shule ya msingi na Hussein Zuberi – shule ya sekondari) wako busy sana kwa sababu sasa mitihani inaendelea, basi ni nzuri kuwasiliana nao tena baada ya wiki mbili. Shule ina wanafunzi wapanda baisikeli 15 na shule ya sekondari ina wanafunzi wapanda baisikeli 70. Mwalimu alisema kwamba ni nzuri kuwafundisha walimu na wapanda baisikeli wanaokaa karibu pamoja na wanafunzi.

Hussein Hamisi alimpa mwanafunzi Kidete Secondary School, Kigamboni barua, na yeye alimpa mwalimu wake. Tutafuatalia zaidi.

Markus na Juma walienda Kigamboni Secondary School na waliwapa barua. Walisema watahesabu kiasi ya wanafunzi wanaopanda baisikeli.

Juma aliwatembelea HUWATA na aliwapa Tsh 50,000 kutoka badjeti ya Wamba ili watumie katika gharama za utawala kutafuta shule. Walitembelea shule nane. Shule tano walisema hawana wanafunzi wanaoenda shuleni na baisikeli (Benjamin Mkapa High School, Msimbazi Mseto Primary School, Diamond Primary School, Upanga Primary School, Olympia Primary School). Shule ya Shaban Robert, Upanga walipenda kushirikiana, pamoja na Mzizima Secondary School, na walikuwa na wazo kufanya shule hizi mbili pamoja kwa sababu wapo karibu. Mbagala Secondary School wanaweza kuwa na wanafunzi wapanda baisikeli 30 lakini watu wa HUWATA walichelewa na hawakutana na mwalimu mkuu.

Markus alikuwa na wazo tuwaalike walimu kushiriki katika training of trainers chuo cha usafirishaji.

Andrew kutoka Ben Bikes na Elaine walikubali kwa email kwamba atakuja hapa tarehe 21 Julai. Sasa tutawasiliana na travel agent wake ili kutayarisha. Tulikubali kuwaambia chuo cha usafirishaji kuhusu tarehe.

**Ofisi**

Ally Saidi Mohammad alipata sehemu pa kukodi lakini chumba kipo ndani sana na haionakani kutoka mtaa. Juma alipata kadiri kutoka fundi kwamba kujenga chumba itakuwa Tsh 700,000 (kazi na vifaa lakini bila mlango). Kadiri hiyo ilisema matofali 300. Hamadi Hatibu Bwaja, ambaye ni fundi wa ujenzi alisema kwamba matofali zaidi yatatakiwa. Tulipima ofisi yetu ya sasa na tulikadiri kwamba ni matofali 700 kwa ajili ya vyumba viwili (moja ya UWABA na moja ya ofisi ya Jumanne), basi hii ni matofali 350 kwa ajili ya kila chumba.

Jumanne alisema kwanza ataongea na mwenye ardhi, halafu hii itasaidia kujua tutapata miaka mengapi bila kodi kwa sababu ya kulipa ujenzi.

**Maswali ya Traffic police, Halmashauri ya Jiji**

Tulifanya orodha ya maswali ambayo bado hatuna majibu:

- Kuna sehemu popote ambapo imeandikwa chini sheria au maelezo ya service roads zaidi ya Road Traffic Act (ambayo haina taarifa ya service roads)? Mfano, sheria ndogo, regulations, dondoo za mikutano, maelezo, karatasi za mafunzo za serekali
- Kama kupaki kwenye service roads hairuhusiwi, kwa nini sheria hii haitekelezwi? (Kawaida kuna magari mengi yamepaki kwenye service roads lakini serekali haifanyi chochote).
- Shirika gani la serekali lina majibu ya kuweka alama za barabara? Inategemea barabara gani (mfano barabara zingine zipo chini ya TANROADS na barabara zingine zipo chine ya serekali za mitaa)?

Tulikubali kwamba Markus na Juma watafuatalia kupata majibu ya maswali haya kutoka traffic police (Bwana Balele) na halmashauri la jiji (Mama Mlamba, engineer wa jiji, mwanasheria wa jiji).

Elaine na Markus walisahau tena kuleta kijitabu walichopata kutoka traffic police.  Paulo alisema ataenda nyumbani kwa Elaine kuandika kwa mkono namba za simu kutoka kijitabu.

**TANROADS**

TANROADS tayari wametoa ahadi (kwa barua) kwamba barabara ya Sam Nujoma na barabara ya Kilwa zitakuwa na njia hasa kwa wapanda baisikeli.  Barabara hizi sasa zinatengenezwa lakini haijulikani njia za baisikeli zipo wapi.  Markus alikubali kupiga picha za barabara na tunweza kuwaonyesha TANROADS na kupata maelezo.

Tulikubali tuandike barua kwenda TANROADS kwa ajili ya kurekebisha shida ya fereji maeneo ya Jangwani barabara ya Morogoro.

**Mambo ya hela**

Elaine na Juma walichukua Tsh 100,000 kutoka benki na Juma aliwapa HUWABA Tsh 50,000 kama badjeti ya Wamba inayosema.  Juma alipata hela ya guta Tsh 7,000.  Yeye na Ally Athman walitumia Tsh 3,000 kwa ajili ya chai na chakula siku walienda Msongole na baisikeli.  Juma alitumia Tsh 500 kufanya photocopy za barua za shule. Sasa ana Tsh 86,000 ya hela ya UWABA nyumbani.